# BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

# TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

## 110 SAYANSI JAMII

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA ........ 1

3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ........ 1

3.1 SEHEMU A: MASWALI MCHANGANYIKO ........ 1

3.1.1 Swali la 1: Kuchagua jawabu lililosahihi ........ 1

3.1.2 Swali la 2: Kuandika Kweli au Sikweli ........ 4

3.2 SEHEMU B: MASWALI MCHANGANYIKO ........ 5

3.2.1 Swali la 3: Kujaza nafasi zilizowazi ........ 5

3.2.2 Swali la 4: Kuoanisha Kifungu ‘A’ na Kifungu ‘B’ ........ 8

3.3 SEHEMU C: MASWALI MCHANGANYIKO ........ 10

3.3.1 Swali la 5: Mada Mchanganyiko ........ 10

3.3.2 Swali la 6: Mada Mchanganyiko ........ 12

2.4 SEHEMU D: MASWALI YA KUELEZEA ........ 15

2.4.1 Swali la 7: Demokrasia ........ 15

3.4.2 Swali la 8: Serikali ........ 18

3.4.3 Swali la 9: Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ........ 20

3.4.4 Swali la 10: Mabadiliko katika utoaji wa huduma za jamii ........ 23

3.4.5 Swali la 11: Shughuli za kiuchumi za Tanzania ........ 25

3.4.6 Swali la 12: Ongezeko la watu na mazingira ........ 27

4.0 HITIMISHO ........ 30

5.0 MAPENDEKEZO ........ 30

VIAMBATANISHO ........ 31

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuingilia Kidato cha Kwanza katika Somo la Sayansi Jamii Mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mitihani ya Kuingilia Kidatu cha Kwanza ni kigezo cha miaka mitatu ya Elimu ya Msingi ambapo wanafunzi hukusudiwa kupimwa ni kwa namna gani wameweza kukumbuka masomo yao ya Darasa la tano (5) hadi la saba (7). Hivyo, mtihani huu ni maandalizi tosha kwa ajili ya Elimu ya Sekondari.

Taarifa inathibitisha sababu ya watahiniwa wengi kupata alama za juu ni pamoja na kuelewa matakwa ya swali husika pia kuwa na kuelewa dhana tofauti juu ya somo la Historia.

Hata hivyo, miongoni mwa sababu kubwa zilizobainika na kupelekea baadhi ya watahiniwa kufanya vibaya ni pamoja na kutojua matakwa ya suala husika, mwandiko mbaya na usiyofahamika na kushindwa kutoa majibu sahihi.

Kwa kuendelea zaidi, uchambuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia machati ambayo yamebainishwa kwa rangi tofauti. Machati hayo yanaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Kwa hiyo, ni imani ya Baraza kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa Elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua kiwango cha ufaulu wa somo la Sayansi Jamii katika Mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa wa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha Taarifa hii.

**Dkt. RASHID .A. MUKKI**



**MKURUGENZI**
**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**
**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa kuingia Kidato cha Kwanza kwa somo la Sayansi Jamii Mwaka 2023. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Zanzibar wa mwaka 2009 na 2022 na kufuata muundo wa mtihani wa Darasa la Saba wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2022.

Mtihani wa Sayansi Jamii ulikuwa na maswali kumi na moja (12) ambayo yalikuwa katika mgawanyiko wa sehemu A, B, C na D. Sehemu A,B ma C zilikuwa ni za lazima ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu A ilikuwa na maswala mawili (2) na sehemu B ilikuwa na maswali mawili (2), Sehemu C ilikuwa na maswali mitatu (3) na Sehemu D ilikuwa na maswali Sita (6) ambapo watahiniwa walitakiwa wachague maswali manne (4).

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **4,442** sawa na asilimia **11.14** ya watahiniwa **39,869** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri ambapo vibaya ulianza alama 0 hadi 20, wastani 21 hadi 60 na vizuri 61 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia chati/grafu kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilisha vibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B, C na D. Pia inawakilisha asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na asilimia ya waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa.

### 3.1 SEHEMU A: MASWALI MCHANGANYIKO

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) kutoka katika mada mchanganyiko. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote mawili (2) ambapo kila swali lilikuwa na alama kumi (10). Hivyo, sehemu hii inafanya jumla ya alama ishirini (20).

#### 3.1.1 Swali la 1: Kuchagua jawabu lililosahihi

Katika swali la 1 watahiniwa walitakiwa kujibu kwa kuchagua jibu sahihi na kuandika herufi ya jawabu katika jadweli iliyotayarishwa. Swali hili limekusudiwa kupima ufahamu na uelewa wa watahiniwa.

**Uchambuzi wa Swali la 1**

Ufuatao ni uchambuzi wa kila kipengele katika swali la moja (1) ambapo lilimtaka mtahiniwa kuchagua jawabu sahihi na kuandika herufi katika jadweli alilopewa.

**Kipengele nambari (i),**

Mtahiniwa alitakiwa kuchagua mwaka ambao Tanzania iliingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Orodha ya jawabu ilikua kama zifuatazo:

A. 1990 B. 1992 C. 1995 D.1999

**Kipengele nambari (ii),**

Kilimtaka mtahiniwa kutaja mwaka rasmi ulioanzishwa Umoja wa Afrika. Kwa kuchagua jawabu zilizoainishwa hapo chini.

A. 2000 B. 2001 C. 2002 D. 2003

**Kipengele nambari (iii),**

Kilimtaka mtahiniwa kutaja wasiokua viongozi wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuangalia jawabu zifuatazo:

A. Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
B. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
C. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar
D. Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania

**Katika kipengele nambari (vi),**

Kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kutaja njia ambayo haihusiani na utoaji wa taarifa za tahadhari. Kwa kutumia jawabu zilizoainishwa hapo chini:

A. Filimbi na mayowe
B. Kukimbia na kilio
C. Kukimbia na kucheka
D. Simu na kilio

**Kipengele nambari (v),**

Mtahiniwa alitakiwa kutaja kati ya malengo ya kuanzishwa Umoja wa Afrika (AU). Kwa kutumia vichachawizi vifuatavyo:

A. India
B. Nchi wanachama
C. Nchi za Ulaya
D. Zanzibar

**Kipengele nambari (vi),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kutaja isiyokua sahihi ya misingi mikuu inayopatikana katika katiba ya Zanzibar. Kwa kutumia orodha ya jawabu zifuatazo:

A. Kuwepo uhuru wa mahakama
B. Mashirikiano baina ya vyombo vya dola na jamii
C. Mgawanyo wa madaraka
D. Usawa mbele ya sharia

**Kipengele nambari (vii),**

Kilimtaka mtahiniwa kutaja lugha ambayo huunganisha nchi za Jumuiya ya Madola. Kwa kuangalia jawabu zifuatazo:

A. Kifaransa
B. Kiingereza
C. Kijerumani
D. Kiswahili

**Kipengele nambari (viii),**

Kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kufahamu maelezo sahihi ya maana ya jinsia. Orodha za vichachawizi ilikua kama ifuatavyo:

A. Hali ya maumbile kwa mwanamke au mwanaume
B. Hali ya maumbile ya wazazi na watoto
C. Mahusiano kati ya familia moja na nyengine
D. Mahusiano ya kijamii kati ya mwanamke na mwanaume

**Kipengele nambari (ix),**

Kilimtaka mtahiniwa kutaja moja kati ya haki za binadamu inayopatikana katika haki za kizazi cha kwanza. Kwa kuangalia orodha za jawabu zifuatazo:

A. Kufanya kazi
B. Kupata elimu
C. Kupata maendeleo
D. Uhuru wa mawazo

**Kipengele nambari (x),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kubainisha miongoni mwa madhara ya rushwa katika jamii. Kwa kuchagua jawabu zifuatazo:

A. Kupata huduma kwa haraka zaidi
B. Kupata maslahi mazuri kwa mfanyakazi
C. Kupatikana kwa maslahi binafsi
D. Kupatikana kwa usalama wa raia

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kujibu maswali mchanganyiko.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,429** sawa na asilimia **99.71** na watahiniwa **13** sawa wna asilimia **0.29** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1a.


**Jadweli nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 908 | 20.50 | 2,952 | 66.65 | 569 | 12.85 | 3,521 | 79.50 |

Takwimu za Jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **66.65** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **79.50**

Aidha, watahiniwa **908** sawa na asilimia **20.50** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1

**Kielelezo 1.1 (Kibaya)**



JAWABU


| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | A | B | C | D | C | D | A | B | A |

Kielelezo 1.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye aliyepata alama mbaya. Mtahiniwa amefahamu matakwa ya swali lakini amekosa vipengele vingi na kupata kipengele kimoja na kupelekea kupata alama 01 katika alama 10. Hii inaonesha ni kushindwa kufahamu maelekezo ya

mtihani na inadhihirisha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na kumbukumbu na uelewa wa kutosha juu ya kile alichoulizwa. Mfano kipengele nambari (i) jawabu ilikua (B) 1992 lakini mtahiniwa alijibu (C) 1995 ambalo sio jawabu sahihi mwaka huo ulifanyika uchaguzi mkuu wa vyama vingi.

Aidha, watahiniwa **569** sawa na asilimia **12.85** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari 1.2

**Kielelezo 1.2 (Kizuri)**


JAWABU

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | C | C | C | B | B | B | D | D | C |

Kielelezo 1.2 ni mfano wa karatasi ya matahiniwa ambaye ameandika majibu sahihi. Majibu hayo yanaonesha wazi kuwa mtahiniwa ana uelewa wa kutosha kuhusu mada alizotahiniwa na ameelewa mahitaji ya swali. Mtahiniwa huyo ameweza kuchagua na kuandika majibu yote sahihi na kufanya kupata alama zote kumi (10) katika swali hilo.

### 3.1.2 Swali la 2: Kuandika Kweli au Sikweli

Katika swali la 2 watahiniwa walitakiwa kujibu kweli kwa maelezo yaliyo sahihi au si kweli kwa maelezo yasiyo sahihi na kuandika herufi ya jawabu katika jadweli iliyotayarishwa. Swali hili limekusudiwa kupima kumbukumbu na uelewa wa watahiniwa. Kwa mtiririrko wa orodha ya maelezo kuanzia kipengele (i-x), na kukamilisha idadi ya alama kumi (10) kama ifuatavyo:

i. Katiba ya kwanza ya Zanzibar iliandikwa mwaka 1984.
ii. Utawala bora huzingatia haki za binadamu na utawala wa sharia.
iii. Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana mamlaka ya kuvunja Bunge.
iv. Mtu anapopata maradhi ya UKIMWI anatakiwa ajitenge na jamii yake.
v. Mfumo wa vyama vingi vya siasa ni mfumo wenye gharama kubwa.
vi. Matumizi ya dawa za kulevya humuathiri mtumiaji na familia yake.
vii. Spika wa Bunge ndiye kiongozi wa shughuli za serikali Bungeni.
viii. Moja kati ya kazi za JKU ni kuzuwia magendo.
ix. Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inajihusisha na uhifadhi wa mazingira.
x. Umoja wa Mataifa ulianzishwa rasmi tarehe 25/9/1945.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kujibu maswali ya kweli au sikweli.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,430** sawa na asilimia **99.73** na watahiniwa **12** sawa na asilimia **0.27** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2a.

**Jadweli nambari 1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 196 | 4.42 | 2,603 | 58.76 | 1,631 | 36.82 | 4,234 | 95.58 |

Takwimu za Jadweli nambari 1b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **58.76** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **95.58.**

Aidha, watahiniwa **196** sawa na asilimia **4.42** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1.

**Kielelezo 2.1 (Kibaya)**

JAWABU

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | K | S | S | S | S | K | K | S | K |

Kielelezo namabari 2.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama za chini. Hii inaonesha kwamba mtahiniwa alishindwa kukumbuka majibu ya kile alichoulizwa na kuandika majibu yasiyo sahihi. Mfano kipengele (i) *katiba ya kwanza ya Zanzibar iliandikwa mwaka 1984* jawabu ni' Kweli' lakini mtahiniwa alijibu 'S' wakati jibu sahihi ni kweli, hii inaonesha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa wa kutosha juu swali husika.

Kwa upande mwengine, watahiniwa **1,631** sawa na asilimia **36.82** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na uelewa wa swali husika kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari 2.2.

**Kielelezo 2.2 (Kizuri)**

JAWABU

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| kweli | Sikweli | kweli | Sikweli | kweli | kweli | Sikweli | Sikweli | kweli | Sikweli |

Kielezo nambari 2.2 ni mfano mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika, mtahiniwa anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha ambaye ameandika majibu sahihi. Majibu hayo yameonesha wazi kuwa mtahiniwa ameelewa vya kutosha juu ya mada alizotahiniwa. Vile vile mtahiniwa ameelewa mahitaji ya swali na kupelekea kupata ufaulu wa juu na kukosea kipengele kimoja (i) kati ya vipengele kumi (x). Mfano kipengele nambari (x) alijibu 'Sikweli' wakati jawabu sahihi ilikua 'Kweli'

**3.2 SEHEMU B: MASWALI MCHANGANYIKO**

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) ambayo ni swali la tatu (3) na la nne (4). Maswali hayo yalikuwa na alama kumi (10) kwa kila moja na hivyo katika sehemu hii inafanya jumla ya alama zote kuwa ni ishirini (20).

**3.2.1 Swali la 3: Kujaza nafasi zilizowazi**

Swali la tatu lilikuwa na vipengele vitano (5) ambavyo ni "a, b, c, d na e" vilivyotoka katika mada tofauti na mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizowazi kwa kuweka jibu sahihi. Majibu ambayo yapo ndani ya jadweli katika karatasi zao za mtihani. Hivyo mtahiniwa alitakiwa achague na kujaza panapohusika kwa usahihi kuanzia kipengele "a hadi e". Kila kipengele kilikuwa na sehemu mbili

zilizokuwa wazi na kila sehemu ilikuwa na alama 01 na kulifanya swali hili kuwa na jumla ya alama kumi (10).

**Kipengele (a),**

Swali lilikua kama, *'Chama cha Afro – Shirazi (ASP) kilianzishwa mwaka 1957 kwa kushirikisha viongozi wa ________ na______________'* Jawabu ilikua Shirazi Association na African Association.

**Kipengele (b),**

Swali liliandikwa kama, *'Huduma za afya wakati wa ukoloni zilitolewa na____________na wakisaidiana na____________'*Jawabu ilikua Serikali ya kikoloni.

**Kipengele (c),**

Swali liliandikwa, *'Mfano wa nchi iliyotumia mfumo wa utawala wa moja kwa moja wakati wa ukoloniAfrika Mashariki ni_______________wakati mfano wa nchi iliyotumia mfumo usio wa moja kwa moja ni___________________'* Jawabu ilikua Kenya na Uganda

**Kipengele (d),**

Swali liliandikwa hivi, *'Miongoni mwa athari hasi za mfumo wa chama kimoja ni ____________ na______________________'* Jawabu ilikua Kukosekana uwazi katika nchi na kudumaa kwa demokrasia.

**Kipengele (e),**

Swali liliandikwa kama**,** *' LudwingKrapf ni miongoni mwa wamishionari kutoka ____________ aliyekuja Afrika kuhubiri amani na upendo. Mmishionari huyo alikuja Zanzibar mwaka _______________'* Jawabu ilikua Ujerumani na 1887.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kujibu maswali ya mada mbali mbali na namna ya kukumbuka alichofundishwa kwa usahihi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,419** sawa na asilimia **99.48** na watahiniwa **23** sawa na asilimia **0.52** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2a.


**Jadweli nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,124 | 25.44 | 2,632 | 59.56 | 663 | 15.00 | 3,295 | 74.56 |

Takwimu za Jadweli nambari 2a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **59.56** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **74.56**

Aidha, watahiniwa **1,124** sawa na asilimia **25.44** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1

**Kielelezo 3.1 (Kibaya)**



Jaza nafasi zilizowazi kwa kuandika jibu sahihi ulilopewa kwenye sanduku.

Ufaransa, Kenya, serikali ya kikoloni, Shirazi Association, Ujerumani, Uganda, African Youth Union, kukosekana uwazi katika nchi, 1844, African Association, Wamishionari, kudumaa kwa demokrasia, 1887, wakunga wa jadi

a) Chama cha Afro - Shirazi (ASP) kilianzishwa mwaka 1957 kwa kushirikisha Viongozi wa Ujerumani na Ufaransa

b) Huduma za afya wakati wa ukoloni zilitolewa na Serikali ya kikoloni wakisaidiana na Kudumaa kwa demokrasia 1887

c) Mfano wa nchi iliyotumia mfumo wa utawala wa moja kwa moja wakati wa ukoloni Africa mashariki ni Wamishionari wakati mfano wa nchi iliyotumia mfumo usio wa moja kwa moja ni 1844


d) Miongoni mwa athari hasi za mfumo wa chama kimoja ni Utawala bora kuzingatia haki za binadamu na utawala wa sheria.

e) Ludwing Krapf ni miongoni mwa Wamishionari kutoka Kenya. aliyekuja Afrika kuhubiri amani na upendo. Mmishionari huyo alikuja Zanzibar mwaka African Assoaation

Kielezo nambari 3.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu swali vibaya ambapo mtahiniwa huyo alijaza nafasi kwa kuandika jawabu zisizo sahihi na ameshindwa kufahamu maelekezo ya swali. Swali lilimtakata achague majibu sahihi lakini majibu aliyoandika siyo sahihi kwa mujibu wa swali. Hii inadhihirisha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa na ufahamu wa mada husika na juu ya alichoulizwa. Mfano kipengele (c) jawabu ilikua Kenya na Uganda lakini yeye alijubu Wamishionari na 1884 hii ilipelekea kupata alama mbaya katika swali husika.

Aidha watahiniwa **663** sawa na asilimia **15.00** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao walifahamu matakwa ya swali na kujibu kwa usahihi kwa kujaza nafasi zote zilizokuwa wazi kama inavyojionesha katika kielelzo namabri 3.2.

**Kielelezo 3.2 (Kizuri)**



3. Jaza nafasi zilizowazi kwa kuandika jibu sahihi ulilopewa kwenye sanduku.

Ufaransa, Kenya, serikali ya kikoloni, Shirazi Association, Ujerumani, Uganda, African Youth Union, kukosekana uwazi katika nchi, 1844, African Association, Wamishionari, kudumaa kwa demokrasia, 1887, wakunga wa jadi

a) Chama cha Afro - Shirazi (ASP) kilianzishwa mwaka 1957 kwa kushirikisha Viongozi wa African Youth Union na African Association

b) Huduma za afya wakati wa ukoloni zilitolewa na Serikali ya kikoloni wakisaidiana na Wamishionari

c) Mfano wa nchi iliyotumia mfumo wa utawala wa moja kwa moja wakati wa ukoloni Africa mashariki ni Kenya wakati mfano wa nchi iliyotumia mfumo usio wa moja kwa moja ni Uganda

d) Miongoni mwa athari hasi za mfumo wa chama kimoja ni Kukosekana uwazi katika nchi na Kudumaa kwa demokrasia

e) Ludwing Krapf ni miongoni mwa Wamishionari kutoka Ujerumani aliyekuja Afrika kuhubiri amani na upendo. Mmishionari huyo alikuja Zanzibar mwaka 1887

Kielelezo 3.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kama inavyotakiwa. Hii inaonekana kuwa mtahiniwa huyu alifahamu vizuri mada alizotahiniwa na kupelekea kupata alama za juu, kwa kupata alama ya vyema katika vipengele vyote (a-e).

### 3.2.2 Swali la 4: Kuoanisha Kifungu 'A' na Kifungu 'B'

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchagua jawabu sahihi kutoka kifungu "B" linalokubaliana na kifungu "A" na kuandika herufi ya jawabu sahihi. Swali lilikua a vipengele vitano (a - e) na kila kipengele cha swali hili lin alama moja (1) na kufanya swali zima kuwa na alama tano (5). Pia swali hili lilitokana na mada ya Umwinyi.

**Uchambuzi wa swali la 4**

Ufuatao ni uchambuzi wa kila kipengele katika swali nambari 4.

**Kipengele (i);**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kujibu usahihi 'Aliteuliwa kukusanya kodi kutoka kwa wakulima' .

**Kipengele (ii);**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kuchagua jawabu sahihi 'Walikuwa wakikodi ardhi kutoka kwa Mamwinyi kwa shughuli za kilimo'.

**Kipengele (iii);**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kujibu kwa usahihi 'Aliteuliwa kumsaidia Mwinyi Mkuu kwa upande wa Unguja'.

**Kipengele (iv);**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kuoanisha kwa usahihi 'Ni mfumo ambao watu wachache humiliki mali kwa manufaa yao binafsi'.

**Kipengele (v);**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kuchagua kwa usahihi 'Aliteuliwa kumsaidia Mwinyi Mkuu kwa upande wa Pemba'.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa ya mtahimiwa katika kuoanisha maelezo yatokanyao na mfumo wa Umwinyi kulingana na vichachawizi walivyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,416** sawa na asilimia **99.41** na watahiniwa **26** sawa na asilimia **0.59** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2b.


**Jadweli nambari 2b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,310 | 52.31 | 1,771 | 40.10 | 335 | 7.59 | 2,106 | 47.69 |

Takwimu za Jadweli nambari 2b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **52.31** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **47.69.**

Aidha, watahiniwa **2,310** sawa na asilimia **52.31** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1.

**Kielelezo 4.1 (Kibaya)**



JAWABU

| KIFUNGU A | i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|---|
| KIFUNGU B | b | A | E | M f | C |

Kielelezo 4.1 ni mfano wa karatasi ya mwanafunzi ambaye ameshindwa kuandika majibu yaliyosahihi kwa mujibu wa mahitaji ya swali. Hii inatokana na kukosa uelewa wa kina juu ya mada aliyotahiniwa na kutokufahamu nini alichotakiwa kufanya. Mfano Kipengele (i) *Aliteuliwa kukusanya kodi kutoka kwa wakulima* Jawabu ilikua 'e' Shakua lakini mtahiniwa alijibu 'b' Nokoa na kupelekea kupata alama mbaya kwasababu alikosa kipengele kizima (i-v)

Aidha, watahiniwa **335** sawa na asilimia **7.59** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao walifahamu matakwa ya swali na kujibu kwa usahihi kwa kujaza nafasi zote zilizokuwa wazi kama inavyojionesha katika kielelzo namabri 4.2.

**Kielelezo 4.2 (Kizuri)**


JAWABU

| KIFUNGU A | i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|---|
| KIFUNGU B | E | h | F | g | A |

Kielelezo 4.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika kwa kuandika majibu yote kwa usahihi. Majibu hayo yameonesha wazi kuwa mtahiniwa ameelewa mahitaji ya swali aliloulizwa.

### 3.3 SEHEMU C: MASWALI MCHANGANYIKO

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) ambayo yalihusisha mada mchanganyiko. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote waliyopewa, swali la tano (5) na la sita (6) yalikuwa na vipengele vitano (5) kwa kila swali. Kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2) na kufanya jumla ya alama kumi (10) kwa kila swali. Hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama ishirini (20). Swali hili lilikusudia kumpima mtahiniwa juu ya uwezo wa kuweza kufikiria na kukumbuka juu ya mada tafauti alizotahiniwa.

#### 3.3.1 Swali la 5: Mada Mchanganyiko

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) (a-e) na liliwataka watahiniwa kujibu kwa ufupi katika sehemu zilizowazi ambapo kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2). Swali hili lilikuwa linapima ufahamu wa mada mbalimbali.

**Uchambuzi wa kila kipengele katika swali nambari 5.**

**Kipengele (a)** kilimtaka mtahiniwa kubainisha faida mbili (2) za msitu wa mkoko kwa jamii ya Zanzibar.

**Kipengele (b)** kilimtataka mtahiniwa kuchora alama inayoonesha i. Daraja na ii. Nyumba.

**Kipengele (C)** hiki kilimtaka mtahiniwa kueleza sababu mbili zinazopelekea visiwa vya Zanzibar huwa na hali ya hewa ya joto kwa muda wa mwaka mzima.

**Kipengele (d)** kilimtaka mtahiniwa kutoa maana ya sensa ya watu.

**Kipengele (e)** kilimtaka mtahiniwa kutaja vyanzo viwili vya maji amabvyo tunavitumia katika maisha yetu ya kila siku.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya mada tafauti kama maswali yalivyoainishwa katika vipengele.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,408** sawa na asilimia **99.23** na watahiniwa **34** sawa na asilimia **0.77** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3a.


**Jadweli nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,397 | 31.69 | 2,619 | 59.42 | 392 | 8.89 | 3,011 | 68.31 |

Takwimu za Jadweli nambari 3a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **59.41** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **68.31.**

Aidha, watahiniwa **1,397** sawa na asilimia **31.69** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1.

**Kielelezo 5.1 (Kibaya)**



5. Jibu kwa ufupi maswali yafuatayo.

a) Bainisha faida mbili (2) za msitu wa mkoko kwa jamii ya Zanzibar.

i. Kituhpatia kuni, mkaa na magongo ya nyumba.

ii. Hutupatia jangwe



b) Chora alama inayoonesha vitu vifuatavyo katika ramani:

i. Daraja

ii. Nyumba

c) "Visiwa vya Zanzibar huwa na hali ya hewa ya joto kwa muda wa mwaka mzima". Kwa kutumia hoja mbili (2) eleza kwa ufupi sababu zinazopelekea hali hiyo.

i.

ii.

d) Nini maana ya sensa ya watu?

Sensa ya watu ni ile hali kuongezeka kwa watu katika matatizo mbalimbali

e) Taja vyanzo viwili (2) vya maji ambavyo tunavitumia katika maisha yetu ya kila siku.


i. Madimbwi

ii. Mfereji

Kielelezo nambari 5.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vibaya kwa kushindwa kuandika jibu sahihi kwa kila kipengele cha swali. Hii inatokana na uelewa mdogo wa mtahiniwa huyo juu ya mada mchanganyiko wa swali hili. Mfano kipengele (e) mtahiniwa alitakiwa *kutaja vyanzo viwili (2) vya maji ambavyo tunavitumia katika maisha yetu ya kila siku. Jawabu ilikua (i) Mito na (ii) Bahari*, lakini mtahiniwa alijibu madimbwi na mfereji na kupelekea kupata alama mbaya katika swali husika.

Kwa upande mwengine, watahiniwa **392** sawa na asilimia **8.89** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao walionekana kuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari 5.2.

**Kielelezo 5.2 (Kizuri)**



5. Jibu kwa ufupi maswali yafuatayo.

a) Bainisha faida mbili (2) za msitu wa mkoko kwa jamii ya Zanzibar

i. Kupata maliasili za misitu na kusababisha upatikanaji wa mvua

ii. Kutengeneza ardhi kuwa imara kwa kupanda mikoko

b) Chora alama inayoonesha vitu vifuatavyo katika ramani:

i. Daraja

ii. Nyumba

c) "Visiwa vya Zanzibar huwa na hali ya hewa ya joto kwa muda wa mwaka mzima". Kwa kutumia hoja mbili (2) eleza kwa ufupi sababu zinazopelekea hali hiyo.

i. Kuwepo kwa mikondo ya bahari hali hii inapeleka kwa Zanzibar na joto au baridi.

ii. Zanzibar ni visiwa ambavyo ni visiwa vikubwa kwa sababu vimezungukwa na bahari.

d) Nini maana ya sensa ya watu?

Sensa ya watu ni kitendo cha kuhesabiwa watu ili kupata idadi maalumu

e) Taja vyanzo viwili (2) vya maji ambavyo tunavitumia katika maisha yetu ya kila siku.

i. Mito ya maji

ii. Visima vya maji

Kielelezo 5.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaoneka kuwa na uelewa wa kutosha juu ya alichoulizwa kupitia mada tafauti.

### 3.3.2 Swali la 6: Mada Mchanganyiko

Swali hili lilimtaka mtahiniwa asome ramani na kisha kujibu maswali yaliyofuata. Swali hili liliku na vipengele vitano **a** mpaka **e** na liliwataka watahiniwa kujibu kwa ufupi katika sehem zilizowachwa wazi ambapo kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2). Swali hili lilikuwa linapi ufahamu wa mada mbalimbali.

**Uchambuzi wa swali nambari 6 kwa kila kipengele**

**Kipengele (a); Mzunguko wa Dunia**

Kipngele hichi kilimtaka mtahiniwa kutaja majina ya mistari ya latitude iliyowasilishwa kwa herufi A na C.

**Kipengele (b); Mzunguko wa dunia**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa Kutaja mabara mawili (2) ambayo yamepitiwa na mstari wa B kwenye mchoro uliowakilishwa.

**Kipengele (c); Mabara na bahari**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kuandika milima miwili (2) mikubwa iliyopo katika bara lililowasilishwa kwa herufi M.

**Kipengele (d); Mabara na bahari**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kutaja majina ya bahari mbili (2) zilizozunguka bara lililowasilishwa kwa herufi M.

**Kipengele (e); Mzunguko wa dunia**

Kipengele hichi kilimtaka mtahiniwa kubainisha athari mbili (2) za mzunguko wa dunia wa masaa 24 (rotation).

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima kumbukumbu na maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya ramani kwa kutumia mchoro uliowakilishwa kwa kutumia herufi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,263** sawa na asilimia **95.97** na watahiniwa **179** sawa na asilimia **4.03** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3b.

**Jadweli nambari 3b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,221 | 52.10 | 1,862 | 43.68 | 180 | 4.22 | 2,042 | 47.90 |

Takwimu za Jadweli nambari 3b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **52.10** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **47.90**

Aidha watahiniwa **2,221** sawa na asilimia **52.10** wamepata ufaulu mbaya.Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1.

**Kielelezo 6.1 (kibaya)**



Chunguza kwa makini mchoro uliopo chini kisha jibu maswali yafuatayo:



a) Taja majina ya mistari ya latitudo iliyowasilishwa kwa herufi zifuatazo:

A: ______________________

C: ______________________

b) Taja mabara mawili (2) ambayo yamepitiwa na mstari wa **B** kwenye mchoro wa hapo juu.

i. Uganda

ii. Tanzania

c) Andika milima mikubwa miwili (2) iliyopo katika bara liliwasilishwa kwa herufi **M**.

i. Kilimanjaro

ii. milima ...

d) Taja majina ya bahari mbili (2) zilizozunguka bara lililowasilishwa kwa herufi **O**.

i. Hindi

ii. Kusi

e) Bainisha athari mbili (2) za mzunguko wa dunia wa masaa 24 (rotation).


i. Kufeti ya mabadiliko ya hewa

ii. Kuchafuka kwa vitu

Kielelezo la 6.1 kinaonesha mtahiniwa aliyefanya vibaya kwa kushindwa kujibu kwa usahihi kwa kila kipengele cha swali. Hii inatokana na uelewa mdogo wa mtahiniwa juu ya mada mbalimbali zilizoulizwa katika swali hili. Mtahiniwa ameandika jawabu zisizofahamika. Mfano kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa ajibu (i) Bara la Afrika (ii) Bara la Amerika Kaskazini lakini mtahiniwa alijibu kinyume cha jawabu sahihi na alijibu (i) Uganda (ii) Tanzania.

Kwa upande mwengine kuna baadhi ya watahiniwa 180 sawa na asilimia 4.22 wamefanya vizuri swali hilo kwa kuweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano vya swali, kuwa mahiri na uelewa wa mada mchanganyiko na ujuzi wa kutosha juu ya swali hilo. Kielelezo nambari 6.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyefanya vizuri.

**Kielelezo 6.2 (kizuri)**



6. Chunguza kwa makini mchoro uliopo chini kisha jibu maswali yafuatayo:



a) Taja majina ya mistari ya latitudo iliyowasilishwa kwa herufi zifuatazo:

– Mstari wa Aktiki

C: Mstari wa ikweta.

b) Taja mabara mawili (2) ambayo yamepitiwa na mstari wa **B** kwenye mchoro wa hapo juu.

i. Bara la Afrika

ii. Bara la Amerika kaskazini

c) Andika milima mikubwa miwili (2) iliyopo katika bara lili... ...lishwa kwa herufi **M**.

i. Mlima wa Kilimanjaro

ii.

d) Taja majina ya bahari mbili (2) zilizozunguka bara lililowasilishwa kwa herufi **O**.

i. Bahari ya pasifiki

ii. Bahari ya Kusini Atlantiki

e) Bainisha athari mbili (2) za mzunguko wa dunia wa masaa 24 (rotation).

i. Mchana na Usiku

ii. ~~Kuwepo kwa mawimbi ya bahari~~

~~Kupanda na k~~

ii) Kuingia na Kutoka kwa maji ya bahari

Ukurasa wa 8 kati ya 16

Kielelezo 6.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri. Mtahiniwa huyu amejibu kwa usahihi kwa kuweza kujaza kwa usahihi vipengele vitano isipokuwa kipengele cha c kitoto cha pili hakuweza kutoa jibu lolote.. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na uelewa mzuri juu ya mada zilizoulizwa katika swali hili pia alifahamu matakwa ya swali.

**2.4 SEHEMU D: MASWALI YA KUELEZEA**

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali sita (6) ambayo yametokana na mada tofauti zikiwemo mada ya Vyama vingi vya siasa, mada ya Serikali, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Huduma za Afya, Shughuli za kiuchumi za Tanzania, Ongezeko la watu na mazingira.

Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali manne (4) na kila swali lilikuwa na alama 10 hivyo katika sehemu hii inafanya jumla ya alama zote ni arobaoini (40).

**2.4.1 Swali la 7: Demokrasia**

Swali hili lilitokana na mada ya ‘Demokrasia’. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza faida mbili (2) na hasara mbili (2) za mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uelewa na maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya kuelezea.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,383** sawa na asilimia **53.65** na watahiniwa **2,059** sawa na asilimia **46.35** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4a.


**Jadweli nambari 4a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,495 | 62.74 | 831 | 34.87 | 57 | 2.39 | 888 | 37.26 |

Takwimu za Jadweli nambari 4a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **62.74** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **37.26**

Aidha watahiniwa **1,495** sawa na asilimia **62.74** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.1.

**Kielelezo 7.1 (Kibaya)** `


7 a ATHARI YA hasara
i Kukosekana Uwazi katika nchi
ii Kudumaa kwa demokrasia
b
i Kupata Kura za mtu nyingi kwa mtu
mmoja
ii Kupata wingi wa kutetea yapi
raia wanaitaka

Kielelezo nambari 7.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kushindwa kujibu swali kwa usahihi na kupelekea kupata alama za chini. Mfano swali lilimtaka kueleza faida na hasara za mfumo wa vyama vingi lakini mtahiniwa alijibu kinyume na matakwa ya swali husika kwa kutoa majawabu kama ilivyobainika

- *Kukosekana uwazi katika nchi*
- *Kudumaa kwa demokrasia*
- *Kupata kura za nyingi kwa mtu mmoja.*

Aidha, watahiniwa Aidha watahiniwa **57** sawa na asilimia **2.39** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.2.

**Kielelezo 7.2 (Kizuri)**

7. JAWABU

Mfumo wa vyama vingi vya siasa ni utaratibu wa demokrasia unaohusisha vyama vingi vya siasa. Mfumo huu umeleta faida nyingi sana katika jamii yetu. Miongoni mwa faida hizo ni kama hizi zifuatazo:-

→ Uhuru wa kutoa maoni. Mfumo wa vyama vingi vya siasa umeleta faida ya wananchi kuwa na uhuru wa kutoa maoni pale ambapo viongozi wa serikali watajadili na kutoa maamuzo kubwa juu ya utekelezaji wa jambo. Hivyo mwananchi akitoa hoja katika kutoa maoni, viongozi watayapitisha na kuyajadili maoni yale. Ndio maana tunasema miongoni mwa faida za mfumo wa vyama vingi vya siasa ni kuwa wananchi kuwa na uhuru wa kutoa maoni.

→ Uhuru wa kuchagua kiongozi na chama. Katika nchi yetu kuna viongozi wengi wa vyama tofauti tofauti kama vile Mheshimiwa Hussein Ali Hassan Mwinyi ambae ni Rais wa chama tawala cha Chama cha Mapinduzi kinachojulikana kwa jina la CCM, Mheshimiwa Tundulisu



chama ambacho wanakipenda watu hao na mwishowe kusababisha mgawanyiko katika jamii.
• Mfumo huu ni wa gharama kubwa, kwa kuwa unapofanyika uchaguzi mkuu ambao hufanyika ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatakiwa kufanyika baada ya kila miaka mitano, pale kununuliwa vifaa vingi vya kupigia kura na vyenginevyo kununuliwa. Pia mfumo huu ni wa gharama kubwa kutokana na watu wengi ni wakaidi (hawaelewi).
Hizi ndizo baadhi ya faida na hasara ambazo ambazo zimejitokeza tu baada ya kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya siasa katika mwaka elfu moja mia tisa na tisini na mbili (1992) na zinajitokeza pale ulipofanyika uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi vya siasa mwaka 1995

Kielelezo 7.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye ameweza kufuata sharia za uandishi wa maswali ya insha na anaonekanwa kuwa na uelewa wa kutosha kama inavyobainika hapo juu.

### 3.4.2 Swali la 8: Serikali

Swali hili lilitokana na mada ya 'Serikali'. Swali hili lilimtaka mtahiniwa Kufafanua kazi nne (4) za Serikali ya Wilaya. Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uelewa na maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya kuelezea.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,188** sawa na asilimia **49.26** na **2,254** sawa na asilimia **50.74** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4b.


**Jadweli nambari 4b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 2 | | WASTANI 2.5 - 6 | | VIZURI 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,898 | 86.75 | 276 | 12.61 | 14 | 0.64 | 303 | 13.25 |

Takwimu za Jadweli nambari 4b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **86.75** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mbaya wa asilimia **13.25.**

Aidha watahiniwa **1,898** sawa na asilimia **86.75** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1.


**Kielelezo 8.1 (Kibaya)**


8-Serikali ni watu au taasisi ndani ya jamii
zenye mamlaka ya kutawala na kupenya
azimio katika nchi. Kuna wilaya mbali
mbali kuna aina mbili za Serikali, nazo ni
i Serikali ya Wilaya
ii Serikali ya Mkoa
-Kuna wilaya mbali mbali hapa Zanzibar
nazo ni
i Wilaya ya Magharibi A Unguja
ii Wilaya ya Magharibi B Unguja
iii Wilaya ya Kaskazini A Pemba Unguja

Kielelezo 8.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amefanya vibaya kwani mtahiniwa aliandika aina za serikali yaani *serikali ya wilaya na serikali ya mkoa pia aliandika wilaya magharibi B na wilaya ya magharibi A kwa upane wa unguja na kaskazini A, badala ya kuandika kazi za serikali ya wilaya.* Hii inaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya serikali pia hakuelewa matakwa ya swali husika.

Aidha, watahiniwa **14** sawa na asilimia **0.64** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyothitisha katika kielelezo nambari 8.2.

**Kielelezo 8.2 (Kizuri)**


8. Serikali ya wilaya ni chombo cha kiutendaji kinachopatikana katika ngazi ya wilaya kinachoisaidia serikali kuu 'ili' kutekeleza majukumu yake. Kuna kazi nyingi katika serikali ya wilaya. Zifuatazo ni kazi tano za Serikali ya Wilaya.

Kuchunguza uhalali wa vitendo na maamuzi ya mamlaka za serikali za mitaa katika eneo lake. Serikali ya Wilaya wanatakiwa kuchunguza kuwa katika wilaya yake kuna ridhamu ya wananchi kupitia ofisi za Sheha.

Kutatua kero za wananchi katika eneo husika kwa vitendo. Katika Serikali ya wilaya wanatakiwa kutatua shinda zote zinazo wakabili wananchi wake kama vile barabara za ndani, umeme wa hospitali na ukarabati wa skuli.

Kutoa huduma kwa mujibu wa viwango na ubora unaotakiwa. Huduma zilizotolewa katika wilaya kama vile usajili wa watoto wanaozaliwa na watu wanaohamia, uhamisho wa wanafunzi.

Kutekeleza majukumu ya kisheria. Serikali ya wilaya wanatakiwa kutekeleza majukumu yote ya msingi ya wananchi wote ambayo yanahusu matatizo ya kisheria kama vile migogoro ya ardhi, wizi wa mazao, mifugo na makosa mengine ya jinai.

Hivyo kutokana na kazi hizo za serikali za wilaya, Serikali kuu inapaswa kutengea rasilimali nyingi za utekelezaji wa kazi hizo. Vile vile wananchi wanapaswa kutoa ushirikiano wa dhati katika utekelezaji wa kazi hizo.

Kielelezo nambari 8.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa aliandika majibu kwa usahihi kulingana na swali husika, hii inaonesha kuwa mtahiniwa ana uelewa wa kutosha juu ya mada husika.

### 3.4.3 Swali la 9: Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

Swali hili lilitokana na mada ya 'Muungano wa Tanganyika na Zanzibar'. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza sababu nne (4) zilizopelekea kuundwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Swali hili lilimpima mtahiniwa jinsi gani Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umeundwa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uelewa na maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya kuelezea.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2, 609** sawa na asilimia **58.73** na **1,833** sawa na asilimia **41.27** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4c.


**Jadweli nambari 4c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,620 | 62.09 | 893 | 34.23 | 96 | 3.68 | 1,023 | 37.91 |

Takwimu za Jadweli nambari 4c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **62.09** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **37.91.**

Aidha watahiniwa **1,620** sawa na asilimia **62.09** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1.

**Kielelezo 9.1 (Kibaya)**


9. Sababu zilizopelekea kuundwa muungano wa Tanganyika ni
Kupata sheria na kanuni.
Kuwa nchi moja
Kupambana vita
Kupata uhuru
Baada ya uhuru yalifanyika mabadiliko ya sekta zifuatazo:-
~~Apya~~ ~~Afe~~ Unyanyasaji haukuwepo
~~Elimu~~ Hati zilitolewa sawa
Hakukua na Ubaguzi

Kielelezo 9.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amefanya vibaya swali husika kuelezea kwa sababu hakuandika maelezo sahihi ya swali husika. Mfano swali lilimtaka kujibu kwa sharia za maswali ya kuelezea lakini alijibu kwa kutumia hoja zisizo sahihi kama inavyobainika.

- *Kufuata sharia na kanuni*
- *Kuwa nchi moja*
- *Kupambana vita*
- *Kupata uhuru*

Aidha, watahiniwa **96** sawa na asilimia **3.68** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyothitisha katika kielelezo nambari 9.2.

**Kielelezo 9.2 (Kizuri)**

9. Sababu zilizopelekea kuundwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Muungano wa Zanzibar na Tanganyika ni kitendo cha kuunganisha nchi mbili huru na kuunda nchi moja ya Tanzania. Kitendo hicho kilifanyika kwa mkataba maalumu baina ya Rais wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika tarehe 26/4/1964. Zifuatazo ni miongoni mwa sababu zilizopelekea kuundwa kwa muungano huo.

Kwanza, kuwepo kwa lugha ya kiswahili, lugha ya kiswahili imekuwa ni nduango muhimu katika kuunganisha muungano huu baina ya nchi mbili huru ambazo ni Tanganyika na Zanzibar pia ili weze kuunganisha nchi hizi mbili kwasababu walielewana kutokana na lugha wanayotumia.

Pia, ukaribu wa kijiografia wa mataifa haya mawili, kutokana na ukaribu wao wa kijiografia wataona bora kuunda nchi moja ambayo ni Tanzania yenye jiografia moja tu.

Vilevile, uendelezaji wa shughuli za biashara na uchumi zilizokuwepo baina ya pande mbili, ili kuweza kuendeleza shughuli za biashara na uchumi zilizokuwepo baina yao ilibidi wawezekuunda nchi hizo mbili iliwe kuwa moja

lililoweza kuendeleza shughuli za biashara na uchumi

Pia, haja ya kuimarisha ulinzi katika eneo la nchi hizi mbili, Ili kuimarisha ulinzi na usalama wa eneo la nchi walitakiwa kuungana ili kuweza kupata watu ambao ni imara ili kulinda nchi, na kama ilivyo kwamba "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu" hivyo iliwabidi waungane ililiweza kupata watu imara wa kulinda nchi.

Mwisho, kuna sababu nyingi zilizopelekea kuweza kuungana nchi hizo mbili hivyo kutokana na sababu hizo tunatakiwa tuweze kuimarisha muungano huo wa nchi hizo mbili na kuwa taifa moja la Tanzania.

Kielelezo nambari 9.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kama inavyobainika.

### 3.4.4 Swali la 10: Mabadiliko katika utoaji wa huduma za jamii

Swali hili lilitokana na mada ya 'Mabadiliko katika utoaji wa huduma za jamii'. Swali hili lilimtaka mtahiniwa alitakiwa kujibu kwa kuchambua mabadiliko manne (4) yaliyojitokeza katika sekta ya Afya. Swali hili lilikusudiwa kumpima mtahiniwa uwelewa na uwezo wa kuchambua mabadiliko ya utoaji wa huduma katika sekta ya Afya mara baada ya uhuru.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uelewa na maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya kuelezea.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,021** sawa na asilimia **45.50** na **2,421** sawa na asilimia **54.50** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4d.


**Jadweli nambari 4d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,261 | 62.39 | 697 | 34.49 | 63 | 3.12 | 794 | 37.61 |

Takwimu za Jadweli nambari 4d zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **62.39** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **37.61.**

Aidha watahiniwa **1,261** sawa na asilimia **62.39** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.1.

**Kielelezo 10.1 (Kibaya)**



10 {4} Mabadiliko yaliyo jitokeza katika sekta ya afya Baada ya uhuru.
i Kuwepo kwa matibabu yaliyoangalia makabila
ii Kuondolo kwa ubaguzi wa rangi katika vituo vya afya
iii Kuondolewa kwa harama mahospitalini.
iv Kuto kuangalia mtako wana adiyo

Kielelezo 10.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amefanya vibaya swali husika na kakuweza kufuata sharia za uandishi wa maswali ya kuelezea na hakuweza kupata alama kwa sababu hakuandika maelezo sahihi ya swali husika. Mfano mtahiniwa alijibu kama ifuatavyo;

- *Kuondolewa kwa matibabu yaliyoangalia makabila*
- *Kuondolewa ubaguzi katika vituo vya afya*
- *Kuondolewa kwa harama mahospitalini*

Aidha, watahiniwa **63** sawa na asilimia **3.12** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyothitisha katika kielelezo nambari 10.2.

**Kielelezo 10.2 (Kizuri)**



10. Mabadiliko manne (4) yaliyojitokeza katika sekta ya Afya ni:

Sekta ya Afya ni sekta ambayo ilifaidika baada ya Mapinduzi bila ubaguzi. na Mabadiliko ya sekta hiyo ni kama:

Kupatiwa matibabu bila ya ubaguzi wowote: hii ilipelekea huduma ya Kijamii kuimarika kwa kwenye sekta ya afya. pia huduma ilipelekea kutobaguliwa dini, rangi wala kabila. mfano kama walivyokuwa wakiwabagua Wakoloni Waingereza.

Kujengwa kwa hospitali ya kisasa: Hii ilipelekea kujengwa kwa mahospitali makubwa kwa ajili ya matibabu au maradhi tofauti mfano wa hospitali hizo ni Allal Abdallah Mzee iliopo Pemba na Jitimai iliopo Unguja.

Kuimarika kwa madaktari wabobezi waliosomea udaktari: Hii pia ilipelekea kuimarika kwa sekta ya Afya kwani tunatibiwa maradhi tofauti mfano, UKIMWI, Homa kali na Kipindu-pindu na hasa hizi za kuambukiza.

Kuongezeka kwa vifaa vingi vya upimaji: Hii ilipelekea kukua kwa sekta ya afya, na vifaa hivyo vilituwasaidia watu mbalimbali hasa wajawazito na watoto wadogo.

Hivyo pia mabadiliko hayo yametusaidia katika mambo mbalimbali pia kutuletea manufaa kwa wananchi na watoto.

Kielelezo nambari 10.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kama inavyobainika.

**3.4.5 Swali la 11: Shughuli za kiuchumi za Tanzania**

Swali hili lilitokana na mada ya 'Huduma za Afya'. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua faida zinazoletwa na sekta ya utalii kwa kutumia hoja nne (4).

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uelewa na maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya kuelezea.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,828** sawa na asilimia **63.67** na **1,614** sawa na asilimia **36.33** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4e.


**Jadweli nambari 4e: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,239 | 43.81 | 1,484 | 52.48 | 105 | 3.71 | 1,641 | 56.19 |

Takwimu za Jadweli nambari 4e zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **52.48** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **56.19.**

Aidha watahiniwa **1,239** sawa na asilimia **43.81** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 11.1.

**Kielelezo 11.1 (Kibaya)**



Sekta ya utalii ina faida nyingi kwa taifa na inaumuhimu kwa sababu huwapa wananchi kipato cha kujiendeleza wenyewe na kwa hilo mi na sema Sekta ya utalii inaumuhimu mkubwa katika taifa.

Kielelezo 11.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amefanya vibaya swali husika na hakufata sharia za uandishi wa maswali ya kuelezea. Mfano mtahiniwa alitakiwa kujibu faida za sekta ya utalii kwa Taifa lakini aliandika kama inavyobainika;

*'Sekta ya utalii ina faida nyingi kwa Taifa na ina umuhimu kwa sababu huwapa wananchi kipato cha kujiendeleza wenyewe na kwa hili mi nasema sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa kwa jamii'.*

Aidha, watahiniwa **105** sawa na asilimia **3.71** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyothitisha katika kielelezo nambari 11.2.

**Kielelezo 11.2 (Kizuri)**



1a Utalii Utalii ni harakati ya watu kwenda mahali
pazuri kwa burudani, biashara au elimu. Kwa hakika
Sekta hii kwa ya utalii imekuwa na faida kwa
taifa. Miongoni mwa manufaa ya sekta hii kwa jamii
ya Zanzibar kama yafuatayo:
Utalii huletea serikali pesa za kigeni. Amb
ayo huipeleka sekta ya utalii kuwa chanzo cha mapa
to serikalini. Watalii wanapoingia nchini mwetu kufanya
utalii basi huingiza kipato serikali kwa kutoa fe
sa za kigeni kwa mamlaka husika ya utalii
na serikali kupata pato lake kupitia kodi inayo
lipwa
Utalii huimarisha uhusiano na mafiki mzuri
baina jamii na watalii. Hii ni pale watalii wana
pokuja nchini kuwa wanataka watu wa kuwasaidia ka
zi pindi wanapokuwepo nchini kwa utalii. Hivyo
hupeleka uhusiano mzuri baina yao.
Utalii huchochea uboreshaji wa njia za usafiri
na mawasiliano. Kama vile hudumu za uwanja wa
ndege wa Abeid Amani Karume, bandari, miundombinu,
na barabara zote za Unguja na Pemba.
Utalii husababisha mseto wa kiuchumi. K
wa kuchangishi shughuli nyingine kupunguza utegeme
zi wa ajira kutoka serikalini nyingine kama vile
madini, usafiri na kilimo
Licha kuwa utalii una faida nyingi kwa jamii
ya Zanzibar lakini pia linakabiliwa na changamoto
kama vile kuporomoka kwa maadili mema na vijambazi

Kielelezo nambari 11.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kama inavyobainika.

### 3.4.6 Swali la 12: Ongezeko la watu na mazingira

Swali hili limetokana na mada ya 'Ongezeko la watu na mazingira' Katika swali hili matahiniwa alitakiwa kueleza hoja nne (4) jinsi ya matokeo ya sensa inavyosababisha uharibifu wa mazingira nchini.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uelewa na maarifa ya mtahimiwa katika kujibu maswali ya kuelezea.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **1,540** sawa na asilimia **34.67** na **2,902** sawa na asilimia **65.33** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4f.


**Jadweli nambari 4f: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,216 | 78.96 | 305 | 19.81 | 19 | 1.23 | 344 | 21.04 |

Takwimu za Jadweli nambari 4f zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **78.96** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **21.04.**

Aidha watahiniwa **1,216** sawa na asilimia **78.96** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 12.1.

**Kielelezo 12.1 (Kibaya)**



- Ongezeko la watu ni kitendo cha kuongezeka
kwa idadi ya watu
Mazingira ni kitu vilivyo tuzunguka sisi
Ongezeko la watu inaweza ikaleta faida au
hasara. Faida ni kama zifuatazo:-
i Mahusiano ya ndoa
ii Kuzaa na kadhalika
Na Hasara ni kama zifuatazo:-
i Kuongezeka kwa vitendo vya ujambazi
na kadhalika
Na pia inasababisha uharibifu wa mazingira
kama vile
i Utupaji wa taka ovyo: Watu wakiwa wengi
taka zinaongezeka na kusababisha maradhi
kama vile Kipindupindu na kadhalika
ii Kuongezeka kwa vitendo vya ujambazi: kila
[illegible] na uhalifu [illegible] kama vile
wizi wa pesha za umma na kadhalika
iii Ongezeko la watoto mitaani: Ikiwa watoto
hawana baba wala mama hutoka na kw-
enda kujitafutia wenyewe riziki
iv Ajira za watoto: Mtoto hushindwa kwenda
shule na kujiingiza katika ajira kwa mfano
Baba na Mama hawana pesha ya kula, [illegible]
[illegible] mashuleni kumtoa, kujiunga
na ajira za watoto ili apate pesa ya kula

Kielelezo 12.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amefanya swali vibaya hakuweza kufuata sharia za uandishi wa maswali ya kuelezea na kupata alama za chini kwa sababu hakuandika maelezo sahihi ya swali husika. Mfano mtahiniwa aliandika kama ifuatavyo;

*Faida za ongezeko la watu ni mahusiano ya ndoa, kuzaa, baba na mama hawana kula ni moja ya sababu ya ongezeko la watu wakati sio mtiririko sahihi wa swali husika.*

Aidha, watahiniwa **19** sawa na asilimia **1.23** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyothitisha katika kielelezo nambari 12.2.

**Kielelezo 12.2 (Kizuri)**

Sensa ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathmini kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemografia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalumu. Zifuatazo ni sababu za uchafuzi wa mazingira.

Uchafuzi wa hewa; Kuongezeka kwa idadi ya watu kumesababisha kuongezeka kwa idadi ya viwanda ambako kunapelekea kwa uchafuzi wa mazingira. Viwanda hivi hutoa kemikali hatari na gesi hewani na kusababisha madhara kwa ubora wa hewa.

Kuenea kwa jangwa. Ni aina ya uharibifu wa ardhi ambapo eneo la nchi kavu tiasi linazidi kuwa kame, kwa kawaida kupoteza maji yake pamoja na mimea na wanyama.

Kupotea kwa bioanuwai. Ukataji miti husababisha upotezaji wa spishi nyingi adimu za kitropiki. uharibifu wa makazi asilia ya spishi nyingi za wanyama na kusababisha upotezaji wa spishi nyingi adimu za kitropiki.

Uharibifu wa udongo; Kuongezeka kwa idadi ya watu kusababisha kuongezeka kwa mahitaji ya uzalishaji wa chakula. Kwa kuwa ardhi ya kilimo katika maeneo mengi wakazi wengi ni ndogo, ardhi ya misitu na ardhi ya asili hubadilishwa kuwa mashamba ambayo huharibu udongo na kusababisha mmomonyoko wa udongo na kufanya ardhi kuwa kavu.

Hivyo basi tunatakiwa tupunguze idadi ya vizazi na atakae haribu mazingira atatakiwa kuwa kulipia faini.

Kielelezo nambari 12.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kama inavyobainika.

**4.0 HITIMISHO**

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali matano (5) yalijibiwa vizuri, maswali sita (6) yalijibiwa wastani na swali moja (1) lilijibiwa vibaya.

Hivyo uchambuzi unaonesha ufaulu mzuri ulipatikana kutokana na uwezo wa watahiniwa katika kufahamu mahitaji ya somo husika, ufanisi na maarifa ya kutosha waliyonayo juu ya mada husika,ufasaha wa kuyachambua maneno waliyonayo yaliyo katika somo la Sayansi Jamii

Pia wanafunzi wengi hawajibu maswali ya kuelezea (Essay question) jambo ambalo linapelekea ufaulu wa chini kwani maswali haya kuanzia swali la 7 hadi 12 yanahitaji uwezo wa kujieleza na yamechukua alama kubwa za mgawanyo wa alama za ufaulu wa chini kabisa wamekuwa na upungufu wa sifa hizo.

Mwisho taarifa hii ya watahiniwa kuhusu ufaulu wa watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Sayansi Jamii na kuondoa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji mada mbalimbali na kuelewa vizuri ili kufanya mwelekeo kwa ajili ya kuongeza ufaulu kwa mitihani mengine ijayo.

**5.0 MAPENDEKEZO**

- Wanafunzi washajihishwe kusoma Historia ya nchi yao na nchi nyengine wakiwa nje ya mazingira ya skuli ili wawe na uwelewa wa kutosha kuhusu Historia kwa ujumla.
- Pia walimu wawafahamishe wanafunzi wao mahitaji ya kila neno la kuulizia swali kama vile elezea, chambua, fafanua, thibitisha, jadili na taja, ili waweze kufafanua vizuri na kupata alama kubwa.
- Walimu wajitahidi kuwafahamisha na kuwashajihisha wanafunzi wao kujibu maswali ya kuelezea kwani wanafunzi wengi wanashindwa kujibu maswali ya kuelezea na wengine wanaacha kabisa na hawajibu hata kidogo maswali hayo ambayo yana alama za juu kabisa.
- Walimu wawazoweshe wanafunzi kujibu maswali yasiyoekewa majawabu hii ni kwa sababu wanafunzi waliowengi wamepata alama za chini zaidi katika maswali ambayo walitakiwa wajaze bila ya kupewa majibu.
- Wazee wawashajihishe watoto wao majumbani wawe na tabia ya kudurusu masomo yao ambayo wamefundishwa shuleni hii itapelekea kuwa na kumbukumbu ya muda mrefu na kuweza kutumia kumbukumbu hiyo katika kujibu mitihani yao.
- Walimu wapewe taaluma na mafunzo ya mara kwa mara ili kuhakikikisha wanasomesha wanafunzi ipasavyo pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kielimu.

**VIAMBATANISHO**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 1**

## UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA KWA MWAKA 2023

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Katiba, Utwala bora, Dawa za kulevya, Demokrasia, Bunge, Ulinzi na Usalama wa Jamii n aTaifa, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Mataifa. | 2 | 95.58 | NZURI |
| 2 | Demokrasia, Umoja wa Afrika, Baraza la Wawakilishi, Katiba, Jumuiya ya Madola, Jinsia, Haki za binadamu, Rushwa. | 1 | 79.50 | NZURI |
| 3 | Harakati za kudai Uhuru Zanzibar, Mabadiliko katika utoaji wa huduma za jamii, Ukoloni katika nchi za Afrika. | 3 | 74.56 | NZURI |
| 4 | Uoto wa asili wa Zanzibar, Ramani, Hali ya hewa, Ongezeko la watu, Vyanzo vya maji. | 5 | 68.31 | NZURI |
| 5 | Shughuli za kiuchumi za Tanzania. | 11 | 56.19 | WASTANI |
| 6 | Mfumo wa Umwinyi. | 4 | 47.69 | WASTANI |
| 7 | Mzunguko wa Dunia, Mabara na bahari. | 6 | 47.90 | WASTANI |
| 8 | Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. | 9 | 37.91 | WASTANI |
| 9 | Mabadiliko katika utoaji wa huduma za jamii. | 10 | 37.62 | WASTANI |
| 10 | Demokrasia. | 7 | 37.26 | WASTANI |
| 11 | Ongezeko la watu na mazingira. | 12 | 21.04 | MBAYA |
| 12 | Serikali. | 8 | 13.25 | MBAYA |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 2**

**UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA KWA MWAKA 2022**

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ulinzi na usalama wa jamii na Taifa, Mahakama, Katiba, Demokrasia, Sheria, Rushwa na Haki za binaadamu. | 2 | 95.44 | NZURI |
| 2 | Mahakama, Baraza la Wawakilishi, Demokrasia, Katiba na Jumuiya ya Madola. | 1 | 89.82 | NZURI |
| 3 | Muungano wa Zanzibar na Tanganyika, Ukombozi wa nchi nyengine za Afrika - Ghana, Zimbwabe, na Msumbuji. Hrakati za kudai uhuru Tanganyika na Ukoloni katika nchi nyengine za Afrika – Kenya, Uganda na Nigeria. | 3 | 84.33 | NZURI |
| 4 | Mabara na bahari, Shughuli za kiuchumi Afrika Mashariki na Ramani. | 6 | 58.31 | WASTANI |
| 5 | Maliasili barani Africa. | 11 | 51.37 | WASTANI |
| 6 | Watu na mazingira. | 12 | 25.97 | WASTANI |
| 7 | Ukombozi wa nchi nyengine za Afrika – Ghana, Zimbabwe na Msumbiji. | 4 | 14.83 | MBAYA |
| 8 | Mfumo wa jua, Mabara na Bahari na Jografia ya Zanzibar. | 5 | 9.28 | MBAYA |
| 9 | Umoja wa Mataifa. | 8 | 8.64 | MBAYA |
| 10 | Jinsia. | 7 | 7.83 | MBAYA |
| 11 | Ukombozi wa nchi nyengine za Afrika. | 9 | 4.40 | MBAYA |
| 12 | Mfumo wa kiuchumi na utawala Zanzibar na Tanganyika hadi 1800. | 10 | 4.30 | MBAYA |